M1

JINA LA MWANAFUNZI : BRITNEY IMANI MZUNGU
PREM NUMBER : 2016 0764965

JINA LA MZAZI | MLEZI : IMANI MZUNGU

ANUANI : S.L.P 90 BIHARAMULO

NAMBA YA SIMU YA MZAZI : 0678070431

MKOA : KAGERA

HARMASHAURI : BIHARAMULO

SHULE YA MSINGI : UMOJA "B" DARASA VI

JINA LA MWALIMU MKUU : KINI M. MUSANA

MWALIMU MKUU
S/M UMOJA 'B'
BIHARAMULO

NAMBA YA SIMU YA MWALIMU MKUU : 0622 568181

M₂ M₁

MBINU ZILIZOTUMIKA KATIKA HARAKATI ZA KUPATA UHURU WA TANGANYIKA

Uhuru ni kujitegemea kwa ujumla au uwezo wa kujitawala kwa kiwango fulani. Tanganyika ilipata uhuru wake mwaka 1961 chini ya utawala wa waingereza wakiongozwa na Richard Turnbul. Chama kilichosaidia kupata uhuru wake ni (TANU) ambacho kilianzishwa tarehe 7 Julai mwaka 1954 kutokana na chama cha (TAA). Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa ni kiongozi wa Tanganyika katika harakati za kisiasa zilizofanikisha Tanganyika kupata uhuru wake. Hadi leo ni miaka 60 tangu Tanganyika ipate uhuru wake.

Baadhi ya mbinu zilizotumiwa na watanganyika katika kudai uhuru wao ni kama hizi zifuatazo: Mbinu za kivita, Vyama vya wakulima, Vyama vya wafanyakazi, migomo, Vyama vya kisiasa na Lugha ya kiswahili.

Mbinu za kivita: Mapigano ya kivita yalitumika kama mbinu ya kudai uhuru wa Tanganyika. Mapambano hayo yalifanywa na baadhi ya makabila ambayo yalikuwa na wapiganaji imara. Mcongoni mwa makabila ambayo yalianzisha mapambano dhidi ya wakoloni ni kama vile: Wahehe chini ya Mtwa Mkwawa, wanyamwezi chini ya Mtemi Isike na Mirambo, Wanyika Mkwawa, wanyamwezi chini ya Mtemi Isike na wamatumbi walishirikiana na makabila mengine ya kusini mwa Tanganyika dhidi ya wajerumani yaliyotokea kati ya mwaka 1905 hadi mwaka 1907.

Vyama vya wakulima: Wakulima walikerwa na mfumo wa kikoloni. Mfumo ambao uliwalazimisha kulipa kodi na kulima mazao ya biashara. Pia, walichukizwa na unyonyaji uliokuwa ukifanywa na wafanyabiashara Wahindi na Waarabu. Vyama hivyo ni kama vile: Chama cha wakulima wa kahawa Kilimanjaro, chama cha umoja wa wahaya Bukoba na shirikisho la Vyama vya shirika vya Nyanza (K.C.U).

Vyama vya wafanyakazi: Wafanyakazi wa kikoloni wenye asili ya Tanganyika walilipwa ujira mdogo ambao haukukidhi mahitaji yao ya kila siku. Pia, huduma za jamii kama vile nyumba zilizotolewa kwa ubaguzi. Nyumba bora walipewa Wazungu, zilizofuatia kwa ubora walipewa Waasia na nyumba duni walipewa Waafrika. Baada ya wafanyakazi kuchoshwa

M

na mfumo wa uchumi wa kikoloni waliamua kuanzisha vyama vya kutetea maslahi yao. Baadhi ya vyama hivyo ni kama vile - Chama cha wafanyakazi, Waafrika Serikalini na shirikisho la vyama vya wafanyakazi Tanganyika.

Migomo: Wafanyakazi na wakulima waligoma kufanya kazi ili wapatiwe haki zao mfano, mwaka 1956 wafanyakazi wa bandari ni Dar es Salaam waligoma kufanya kazi mpaka watekelezewe madai yao kama vile kulipwa ujira mzuri.

Vyama vya kisiasa: Vyama vya wakulima na wafanyakazi havikufanikiwa kuleta uhuru na ukombozi wa kweli. Hivyo walianzisha vyama vya kupigania uhuru wa kweli. Vyama hivyo vilikuwa na wanachama kutoka jumuiya ya wakulima na wafanyakazi. Baadhi ya vyama hivyo ni kama vile: Chama cha Waafrika (African association - AA) kilichoanzishwa Dar es Salaam mwaka 1929 na baadaye kilianzishwa Zanzibar mwaka 1934.

Lugha ya kiswahili: Watanganyika walitumia lugha ya kiswahili katika kuwasiliana hivyo kuwaunganisha katika harakati za kudai uhuru wao. Mfano, Watanzania walitumia lugha ya kiswahili katika vita na hivyo kuwafanya kuweza kuelewana.

Mbinu zote zilizoelezwa hapo juu ndizo zilizotumiwa na watanganyika katika kupata uhuru wao 9/12/1961 chini ya chama cha (TANU) kikiongozwa na mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kwa hiyo hatuna budi kudumisha amani, umoja na mshikamano katika taifa letu.